MMUST PUBLISHING PRESS

Jarida la Kiswahili Sanifu

# Ufasiri Mpya wa Maana za Methali za Kiswahili katika Diskosi za Kizazi cha Gen Z kwenye Mtandao wa Tiktok, Kenya

Lina Akaka [1] Mwaniki Mugwe [2]

[1]Chuo Kikuu cha Kirinyaga, Kenya

[2]Chuo Kikuu cha Embu, Kenya

**IKISIRI**

**Ikisiri**

Makala hii inaangazia jinsi kizazi cha Gen Z hubuni upya methali asilia za Kiswahili kwa kuongeza au kubadilisha maneno ili ziwiane na uhalisia wa miktadha ya sasa. Hali hii hupoteza jgmaana zilizokusudiwa za methali asilia pamoja na uzito wa hekima iliyomo. Mabadiliko hayo huibua ucheshi na kukejeli hekima ya pamoja ya jamii. Kwa misingi hii, makala imechunguza jinsi ubunifu huo mpya unavyosababisha mabadiliko ya maana, maneno yaliyomo na kuongeza vifungu vya maneno katika methali za kimapokeo ili ziwiane na miktadha mipya zinamotumika. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Baada-Usasa kwa mujibu wa Lyotard (1984). Muundo wa utafiti ni wa kimaelezo. Eneo la utafiti ni mtandao wa kijamii wa Tiktok, Kenya na eneo la kitaaluma ni fasihi simulizi. Data za msingi zilikusanywa kwenye mtandao wa kijamii wa Tiktok, Kenya na maktabani ambako data za upili zilikusanywa. Sampuli ya utafiti ni baada-methalijadi za Kiswahili. Baada-methalijadi 20 zilikusanywa. Baada-methalijadi 8 ziliteuliwa kimaksudi na kuchunguzwa. Data za methali za kimapokeo zilichanganuliwa pamoja na kila baada-methalijadi iliyotokana nazo. Mabadiliko ya kimaana, kimuundo na kimuktadha ya kila methali yalijadiliwa huku watafiti wakirejelea maoni ya watafiti wengineo kuhusu methali hizo mpya. Matokeo ya utafiti yalifichua kuwa vijana wa kizazi cha Gen Z hubadilisha muundo na maana za methali za kimapokeo ili kukidhi haja za uhalisia wa miktadha ya sasa.

**KUHUSU MAKALA**

*Maneno Muhimu:*
Baada-methalijadi, Methali asilia, Methali za Kimapokeo, Kizazi cha Gen Z

*Historia ya Makala:*
Tarehe ya Kutumwa:8 Mei 2026
Tarehe ya Kurekebishwa:6 Julai 2026
Tarehe ya Kukubalika:7 Juali 2026
Mtandaoni: 26 Agosti 2026

*Mwandishi Mkuu. Simu: +254720929733; Barua Pepe lakaka@kyu.ac.ke

Mhariri: Frida Miruka, Chuo Kikuu cha Masinde Muliro, Kenya.

Nukuu: Akaka, L & Mugwe, M (2026). Ufasiri Mpya wa Maana za Methali za Kiswahili katika Diskosi za Kizazi cha Gen Z kwenye Mtandao wa Tiktok, Kenya. Jarida la Kiswahili Sanifu 3(2), 43-49

© 2026

Creative Commons Attribution License (CC BY-NC-SA)

## 1. Utangulizi

Methali kama kipengele cha maarifa ya kiasili zimekitwa katika shughuli za jadi za wenyeji. Maarifa ya kiasili hutoa uelewa wa kina wa utamaduni wa jamii na kuhakikisha utangamano na umoja wa tamaduni, (Ogbebor, 2011). Kulingana na Kim na wenzake (2017), methali hufumbata tajriba za maisha ya wanajamii na miono-ulimwengu yao. Methali za Kiswahili ni hazina muhimu ya maarifa ya kutamaduni, mwongozo wa maadili na kaida za kijamii ndani ya jamii zinazozungumza Kiswahili. Methali zinatambuliwa kote kama maelezo mafupi ya hekima inayoshirikiwa kwa pamoja ambayo hupitisha thamani za jadi kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kulinagana na Finnegan (2012), methali zina jukumu muhimu la kuhifadhi tajriba za jamii na kuelekeza tabia za kijamii kupitia kwa sitiari.

Kihistoria, methali za Kiswahili zilikuwa zikitamkwa kimamlaka kama hekima ya kijamii, kaida za kijamii na kwa minajili ya ushauri wa maadili. Egbara (2020) anasema methali za jadi zilithaminiwa kwa sifa zake za ushawishi na kutumiwa katika mazungumzo ili kuelimisha, kushauri au kuimarisha matarajio ya jadi. Mamlaka zilizobeba methali hizi yalitokana na wahenga pamoja na wazee, na maana zake zilifahamika na kutambuliwa na wanajamii. Maana ziliimarika, hazikubadilikabadilika. Hata hivyo, vijana wa sasa hususan wa kizazi cha *Gen Z* wamekuwa wakizibadilisha kiubunifu katika diskosi zao. Aghalabu hubadilisha maana zikawa za kuchekesha, kukejeli au kuakisi masuala ya kijamii. Mwelekeo wa kizazi cha *Gen Z* wa kubadilisha maneno katika methali unaonyesha kuwa methali sio turathi za jadi zisizobadilika ila ni maumbo yanayobadilika ambayo yanaweza kuundwa na kufasiriwa upya kulingana na miktadha ya kijamii inayobadilika, (Fadare, 2020). Katika uchanganuzi wake wa baada-methalijadi, Raji-Oyelade (1999) aliasisi dhana ya *postproverbials (*baada-methalijadi- tafsiri yetu) ili kufafanua mabadiliko na mapinduzi katika methali za kimapokeo. Baada-methalijadi ni methali zilizotokana na methali za kimapokeo na zikaundwa upya kwa kubadilisha muundo, maana na matumizi ili zikidhi diskosi za miktadha ya sasa. Baada-methalijadi huwakilisha namna mojawapo ya shughuli za kiujumi ambapo wazungumzaji hudengua kiubunifu misingi iliyowekwa ya methali kwa kutumia kejeli, kupindua utaratibu wa maneno na maana (Raji-Oyelade na Oyeleye, 2019).

Egbara (2020) anasema baada-methalijadi ziliibuka wazungumzaji walipoanza kufaragua methali ili kuunda mpya lakini zinazohusiana na zile za kimapokeo. Isitoshe anadai maana ya baada-methalijadi hutegemea jinsi hadhira inavyotambua methali ya kimapokeo iliyofaraguliwa. Anaendelea kufafanua kwamba, bila ufahamu wa methali ya kimapokeo, ucheshi au fasiri mpya inaweza kupotoshwa kwa kuwa hizi methali za sasa hutegemea maarifa ya jadi yanayoshirikiwa kwa pamoja, utambuzi wa mwingiliano matini na ufahamu wa pamoja wa methali za kimapokeo.

Kutokana na mawazo ya Egbara (2020) methali za kimapokeo huwa kama msingi ambamo baada-methalijadi huundwa. Methali za kimapokeo huwa kama mzizi wa hizo mpya kwa kuwa haziwezi kufahamika bila hizo za jadi, ni kama vimelea vya methali za kimapokeo.

Licha ya kwamba, kizazi cha *Gen Z* kinaonyesha hali ya juu ya ubunifu kilicho nao, hali hii kama anavyodai Adom na wenzake (2021) inatishia kuangamiza methali za kimapokeo ambazo ni mojawapo ya mifumo ya maarifa ya jadi yenye mizizi yake katika falsafa ya Kiafrika. Badala ya kutumikiza methali kama ukweli mtakatifu usiobadilishwa ambao jamii imepokea kutoka kwa wahenga, wazungumzaji wa kizazi kipya huzibadilisha kiutani na kuzalisha maana mpya ambazo huakisi tajriba na mielekeo ya sasa. Fadare (2020) anahoji kuwa mabadiliko kama hayo huonyesha uwezo wa simulizi za Kiafrika kufaraguliwa kiwakati. Jambo hili linadhihirisha namna simulizi za jadi zilizorithiwa zinavyoweza kubadilika na kutumika katika mazingira yanayobadilika ya kijamii na kiisimu. Anaendelea kueleza kuwa, hivyo baada-methalijadi hufanya kazi kama miundo ya kiisimu iliyovumbuliwa kutokana na hekima ya jadi huku ikipinga au kufasiri upya mamlaka yake katika diskosi za sasa. Raji-Oyelade (1999) anaeleza baada-methalijadi hutamkwa kiutani katika diskosi za kawaida kwa kuvuruga maana na mpangilio wa maneno ulivyo katika methali za kimapokeo. Katika muktadha wa Kiswahili, mabadiliko haya yanabainika sana miongoni mwa wazungumzaji wa kizazi cha *Gen Z* ambao huziunda methali za kimapokeo upya wanapowasiliana.

Kuna sababu kadha wa kadha za kiisimujamii na kitamaduni zinazofanya vijana wa kizazi cha *Gen Z* kupendelea baada-methalijadi badala ya methali za kimapokeo. Mabadiliko yaliyopo katika methali zinazobuniwa na kizazi hiki yanaakisi jinsi lugha inavyoweza kubadilika ili kuwiana na uhalisia mpya wa kijamii. Baadhi ya mabadiliko hayo yanasababishwa na usasa, athari za miji na elimu ya Magharibi kama wanavyodai Raji-Oyelade na Oyeleye (2019**)**. Methali za kimapokeo zilibuniwa katika jamii za kilimo na ujamaa ilhali kizazi cha *Gen Z* kinaishi katika miji, udijitali na mazingira ya utandawazi. Methali nyingi za kimapokeo zinarejelea kilimo, wanyama, maisha ya vijijini na utawala wa jadi. Kwa hivyo *Gen Z* huzibuni upya ili zilingane na tajriba zao za sasa kama vile teknolojia, mahusiano na tajriba zao za maisha ya mijini. *Fadare (2020) anashadidia wazo hilo anaposema vijana, ambao ni watumiaji wengi wa mitandao ya kijamii hudengua methali za kimapokeo na kuzibuni upya ili ziwiane na miktadha ya sasa*. Isitoshe *Gen Z* pia hupendelea kubuni na kufanyiana utani.

Mawasiliano baina ya vijana wa kizazi cha *Gen Z* hugubikwa na ucheshi, ujasiri na utani wa kuvuruga miundo iliyozoeleka ya maneno. Hivyo kwa kufanya hivyo, *Gen Z* hubadilisha miundo ya methali ili kukejeli hekima ya jadi, kufanya mizaha na kuburudisha wasikilizaji (Egbara, 2020). Hivyo methali hizo zinakuwa vifaa vya ucheshi kuliko miongozo ya maadili. *Gen Z* hubuni upya methali za kimapokeo pia katika jitihada za kujenga utambulisho wa kizazi chao. Ubunifu huo mpya huwatofautisha na kizazi cha wazee kando na

kubuni mtindo wao wa kuwasiliana na kuonyesha kwamba utamaduni umebadilika. Methali walizobadilisha pia huakisi ukaidi wa kaida za jadi kwa kukejeli au kupinga mamlaka ya wazee, majukumu ya kijinsia na matabaka ya kijamii kama yanavyoakisiwa katika methali za kimapokeo.

Makala hii ilichunguza uibukaji wa baada-methalijadi katika mazungumzo ya kizazi cha *Gen Z* kwa kuchunguza jinsi vijana wa kizazi hicho hubuni upya methali za kimapokeo kupitia kwa mabadiliko ya kimaana, mpinduo wa utaratibu wa maneno na fasiri za kiutani. Hali hii imebainisha jinsi methali za Kiswahili huwekwa kwenye miktadha mipya na kuhuishwa ili kuakisi uhalisia wa mabadiliko ya jamii kitamaduni na kijamii.

## 2. Mapitio ya Maandishi

Katika sehemu hii, waandishi watapitia tafiti, makala na kazi nyinginezo zilizotangulia ambazo zinahusiana na utafiti huu ili kuunganisha nazo. Kwa kufanya hivyo, utafiti huu utaunda msingi wa utafiti na kuuweka katika muktadha mpana wa mjadala wa kitaaluma. Utahalalisha pia umuhimu wa kufanyika kwa uchunguzi zaidi.

Omari (2016) alichunguza namna waandishi wa fasihi ya Kiswahili na watumiaji wa mitandao ya kijamii wanavyoshiriki katika uundaji na usambazaji wa methali za sasa za Kiswahili nchini Tanzania. Omari anasema baada-methalijadi ni miundo iliyobuniwa upya kutokana na methali za kimapokeo ambazo zimepinduliwa, kupanuliwa au kuundwa upya ili kuzalisha maana mpya. Omari anadai miundo hii mipya ya methali aghalabu hukanusha, kukejeli au kudhihaki hekima ya methali asilia ya kimapokeo kupitia kwa mikakati ya kiisimu kama vile kuvuruga, kuongeza vifungu au kufupisha. Mabadiliko haya huibuka kutokana na hali za kijamii na kitamaduni zinazobadilika zikiwemo utandawazi, maendeleo ya teknolojia na uhalisia wa mabadiliko ya kisiasa na kitamaduni. Hivyo zinaakisi mchakato wa udenguzi na uundaji upya wa maarifa ya jadi na kupinga mamlaka, umuhimu na ukweli uliomo. Utafiti wa Omari (2016) hauna tofauti kubwa na utafiti huu, ulichunguza vipengele vilivyochunguzwa ila tofauti inatokea katika methali za kimapokeo zilizochunguzwa na miktadha iliyozalisha maana mpya za methali hizo.

Raji-Oyelade na Oyeleye (2019) walichunguza dhana ya baada-methalijadi na uhuru wa kubadilisha methali za kimapokeo ili kuakisi miktadha ya sasa. Utafiti wao ulilenga kubaini jinsi methali za kimapokeo hubadilishwa kiubunifu katika diskosi za sasa. Nadharia zilizoongoza utafiti wao ni za Baada-Usasa na Baada-Umuundo. Walihoji kwamba baada-methalijadi ni fasiri za kiutani za methali za kimapokeo ambazo huvuruga maana za jadi zilizofahamika kupitia kwa vichekesho, kejeli na uvumbuzi wa maneno kiubunifu. Matokeo ya utafiti wao yalidhihirisha ubadilikaji wa simulizi za jadi za Afrika na kuonyesha vile maarifa ya jadi yanavyoendelea kufasiriwa upya katika miktadha tofauti.

Adom na wenzake (2021) walichunguza methali za Kiafrika kama chombo cha maarifa ya kienyeji na elimu ya jadi na kutalii njia ambazo zingehifadhiwa kidijitali kwa ajili ya vizazi vijavyo. Utafiti wao ulijadili pia mabadiliko na ufasiri mpya wa methali za kimapokeo katika mawasiliano ya sasa. Katika utafiti wao, waliangazia jinsi vijana wanavyobadilisha methali za kimapokeo ili zisawiane na miktadha ya sasa. Nadharia ya ethino-pragmatiki iliongoza utafiti wao. Matokeo ya utafiti wao yalifichua kwamba hata ingawa methali zinasalia kuwa rasilimali muhimu za jadi, zinatishiwa kupotea na usasa pamoja na kupungua kwa matumizi yake miongoni mwa vizazi vichanga. Utafiti huu ulibaini kuwa hali hii katika mitandao ya *Tiktok* nchini Kenya inaonyesha methali zingali zinatumiwa sana isipokuwa, umbo lake la kimapokeo ndilo limo katika hatari ya kubadilishwa.

Utafiti wa Nnabuihe (2024) ulichunguza jinsi methali teule za Kiigbo zinavyobadilishwa hadi baada-methalijadi kwa kutalii tofauti, sababu za mabadiliko hayo, mielekeo ya jamii na athari za jadi za hii miundo mipya. Utafiti wake ulichukua mtazamo wa kiisimu-anthropolojia. Baada ya mahojiano na wazee pamoja na vijana, utafiti wake ulitambua kwamba baada-methalijadi huakisi mabadiliko ya kijamii, utandawazi na mitagusano baina ya watu kutoka tamaduni tofauti huku wazee wa Kiigbo wakipendelea methali za kimapokeo na vijana wakipendelea methali zilizobuniwa upya na kusasishwa ili zilingane na miktadha ya hali ya maisha ya sasa. Hali katika jamii ya Waigbo ni sawia na hali iliyopo kwenye mtandao wa *Tiktok* nchini Kenya. Vijana wanapendelea methali zilizobuniwa upya huku wazee wakidumisha matumizi ya methali jadi.

Ojiakor (2024) alichunguza vile methali za kimapokeo za Waigbo zinavyobadilishwa na kuwa baada-methali jadi. Anadai kwamba hizi methali mpya hubeba hekima mpya inayotokana na mabadiliko ya utamaduni. Ojiakor anachunguza jinsi methali vipengele vya utamaduni wa sasa huingizwa katika methali za Kiigbo na kubadilisha msamiati ili matumizi yake yawiane na miktadha ya sasa. Hivyo, anahoji Ojiakor kwamba vipengele vilivyoingizwa, huungana na hekima ya kale iliyomo katika umbo asilia ya methali pamoja na muktadha mpya zinamotumiwa na kuiimarisha hata zaidi. Hali hii ni inatofautiana sana na methali

zinazochunguzwa katika utafiti huu ambazo zimesheheni chuku, vichekesho na kejeli kinyume na baada-methalijadi za Kiigbo ambazo zinaendeleza hekima na mafunzo ya methali jadi za jamii hiyo. Nadharia ya Baada-Ukoloni iliongoza utafiti wake. Matokeo ya utafiti wake yanadhihirisha kwamba baada-methalijadi huibuka kwa sababu ya tajriba ya utawala wa kikoloni, utandawazi na uhalisia wa sasa wa kijamii, hivyo utamaduni hubadilikabadilika sio tisti kama jiwe. Hata hivyo katika uchunguzi wake aligundua kuwa baada-methalijadi zinahusiana sana na methali za kimapokeo kimuundo na kimaana ila muktadha zinamotumiwa ndio hubadilka.

Adeniyi na Ojerinde (2024) walichunguza baada-methalijadi katika Kipijini cha Nigeria, uhalisia wa kijamii uliosimbwa ndani ya baada-methalijadi hizo na majukumu yake ya kiisimu na utamaduni katika jamii. Nadharia ya Isimujamii iliongoza utafiti wao. Matokeo ya utafiti wao yalionyesha kwamba methali hizo zimekitwa sana katika tajriba za maisha ya wanajamii na zinaakisi uhalisia wa Nigeria ya sasa. Methali hizi zinapoibuliwa, huenea haraka na hueleweka na kushadidiwa na jamii. Wanajamii huzitumiwa kuhakiki mamlaka, kueleza kuhusu masuala yanayoikumba jamii bila kuzua fujo hivyo kuwa vifaa salama vya kuhakikia jamii. Jambo hili linatokea pia katika methali zinazochunguzwa katika utafiti huu. Vijana huzitumia kuhakiki wanasiasa na masuala mbalimbali yanayoikumba jamii. Maoni ya Adeniyi na Ojerinde kuhusu methali hizi za sasa ni kwamba zimebuniwa upya kutokana na methali za kimapokeo na hudumisha uhusiano nazo, sawia na methali zinazochunguzwa. Methali hizo huakisi mapambano katika maisha ya kila siku, matatizo ya kiuchumi na ufisadi, hivyo hupendelewa na kutumiwa sana miongoni mwa watu wa tabaka la chini.

## 3.0 Msingi ya Kinadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Baada-Usasa kwa mujibu wa Lyotard (1984). Mawazo ya Lyotard kuhusu baada-usasa yaliwekwa misingi na Nietzsche (1968) na Heidegger (1962). Wananadharia hawa walipinga falsafa ya Kimagharibi ya kupendelea ukweli bia na mantiki. Walihoji kwamba maana ilifungamana na maisha ya binadamu pamoja na muktadha, sio mifumo bia. Kutokana na misingi hiyo, Lyotard, kupitia kwa kitabu chake cha semina chenye anwani '*The Postmodern Condition: A Report on Knowledge*' (*La Condition postmoderne*) alianzisha wazo maarufu kwamba baada-usasa umekumbwa na shaka kuhusu simulizi zinazodai kueleza kila kitu.

Kuanzia mwaka wa 1979, uchunguzi na ufafanuzi wa nadharia ya baada-usasa ulifanywa kwa uwazi kwa kuihusisha na maarifa, sayansi na uhalali wa ukweli. Baadaye Hutcheon (1988) aliipanua zaidi nadharia hiyo kwa kudai kuwa baada-usasa hauiachi historia, unaifasiri upya kiuhakiki. Jameson (1991) aliijenga zaidi nadharia ya baada-usasa alipohoji kwamba ni zao la ubepari wa sasa. Alieleza kwamba tamaduni mbalimbali katika enzi hizi za baada-usasa zinaakisi uhalisia wa miundo iliyopo ya kiuchumi na kijamii badala ya ubunifu wa kiujumi.

Lyotard (1979) alidai hakuna jamii iliyoamini kikamilifu katika ukweli bia, mila au maana zisizobadilika. Aliibua mihimili saba ya nadharia hii ikiwemo utupiliaji mbali wa simulizi zinazofahamika, fasiri mpya ya maana, matumizi ya michezo ya lugha, thamani ya utendakazi wa simulizi kuliko ukweli, udenguzi wa mamlaka, mwingiliano matini na miktadha mipya, matumizi ya mizaha, chuku na upinzani. Hii mihimili yote iliwafaa watafiti katika uchanganuzi wa data za methali zilizokusanywa.

## 3. Mbinu za Utafiti

Muundo wa utafiti huu ulikuwa wa kimaelezo. Eneo la utafiti lilikuwa mtandao wa kijamii wa *Tiktok, Kenya* ambako data msingi zilikusanywa na maktabani ambako data za upili zilikusanywa. Kundi lengwa la utafiti lilikuwa methali za Kiswahili na sampuli ya utafiti lilikuwa methali za kimapokeo na baada-methalijadi za Kiswahili. Baada-methalijadi 20 zilikusanywa kwenye mtandao wa kijamii wa *Tiktok* na baada-methalijadi 8 zikateuliwa kimaksudi kwa misingi ya ukiushi wa kimuundo uliomo, vinyume na utajiri wa uhalisia wa maudhui yaliyomo ili kutafitiwa. Methali za kimapokeo ambazo baada-methalijadi zilizotafitiwa zilitokana nazo zilitambuliwa na kuchanganuliwa pia. Aina zote mbili za methali zilisimbwa kwa nambari na herufi; methali za kimapokeo zikisimbwa kama Methali$^{1a}$, Methali$^{2a}$, Methali3a na kadhalika huku vimelea vyake vikisimbwa kama Methali$^{1b}$, Methali$^{2b}$, Methali$^{3b}$ na kadhalika. Data zilichanganuliwa kwa kunakili methali za kimapokeo katika daftari na kuchunguza utaratibu wa maneno, maana za kimapokeo zilizomo na matumizi yake ya jadi. Hatimaye, mabadiliko yaliyojitokeza katika kila methali ya kimapokeo yalifasiriwa na kujadiliwa kwa kuongozwa na nadharia ya utafiti.

## 4. Uchanganuzi wa Methali

Baada-methalijadi ni methali za kimapokeo zilizobuniwa upya ambapo wazungumzaji hubadilisha kimaksudi elementi za methali asilia ili kuzalisha maana zinazoakisi uhalisia wa jamii ya sasa (Egbara, 2020). Watafiti walipanga sehemu hii katika mada ndogondogo za methali za kimapokeo ambazo zimesimbwa kwa alama Methali[1a,] Methali[2a,] Methali[3a] na kadhalika. Aidha baada-methalijadi zimesimbwa kwa alama Methali[1b], Methali[2b] na Methali[3b.] Maana za ndani na nje za methali za kimapokeo zilichunguzwa. Hatimaye matumizi yake ya kitamaduni yalielezwa. Mabadiliko ya methali hizi yalichanganuliwa kwa misingi ya muundo, mpangilio wa maneno, maana na matumizi yake katika miktadha ya sasa kama ilivyobainishwa katika sehemu ifuatayo.

### 4.1.1 Methali[1a]: Akili ni mali

King'ei na Ndalu (2008) wanaeleza maana na matumizi ya methali hii. Wanafafanua kuwa kila mtu mwenye kutumia akili yake ipasavyo atajipatia pato au mali. Methali hii inahimiza na kushauri watu watende mambo kwa busara au hekima. Muundo wake ni sahili wenye tamko fupi. Tamko hili ni funge pia na lenye mamlaka. Maana inayojitokeza ni kwamba akili ni mtaji wenye thamani. Methali inasisitiza maarifa, hekima na urazini ni rasilimali ya kudumu. Muktadha wa matumizi ya methali hii ulikitwa katika hekima za jamii ya Kiafrika, hivyo inaakisi maadili thabiti na imani kwamba maarifa ni nguvu. Katika umbo lake la kimapokeo, methali hii ni thabiti, ni ya kijamii na imekitwa kwenye maadili. Vijana wa kizazi cha *Gen Z* wameibuni upya methali hii kwa kutumia kinyume na kuongeza neno ambalo halipo katika methali asilia ya kimapokeo kama ifuatavyo:

### 4.1.2. Methali[1b]: Wahenga hawaamini akili si mali tena

Methali hii inapinga hekima ya wahenga. Inasema akili si mali tena. Hali hii inawiana na mawazo ya Lyotard (1984) katika nadharia ya baada-usasa kwamba jamii ya sasa hupinga ukweli uliokuwa ukikubalika katika jamii za jadi. Kwa mfano, katika muktadha wa kitamaduni, dhana akili katika methali hii inawakilisha maarifa. Hivyo, vijana wa sasa wanafasiri maarifa hayo kuwa ya kielimu, ndio maana wameibadilisha na kusema wahenga hawaamini akili si mali tena. Wanahusisha akili na kuelimika. Hivyo wanaonyesha kwamba akili aliyo nayo mtu katika maisha inaweza kumtajirisha bila kuelimika. Vijana wa kizazi cha *Gen Z* wana njia nyingi za kutengeneza hela zisizohitaji mtu kuwa ameelimika ili atajirike. Kwa muda mrefu, elimu imekuwa ikionekana kama ufunguo wa maisha mazuri yenye ustaarabu. Hata hivyo, vijana wamebuni njia mbadala za kujipa kipato kando na kuichukulia elimu kama ufunguo wa maisha ya ustaarabu.

Muktadha wa toleo jipya la Methali[1a] ni wa sasa ukilinganishwa na muktadha wa methali hiyo katika umbo la kimapokeo. Baada-methalijadi huibuka wazungumzaji wanapobadilisha, kupanua, kuiga au kuunda upya methali za kimapokeo ili ziwiane na muktadha wa sasa (Ajadi na Oloruntoba-Oju, 2023). Kwa muda mrefu, elimu imekuwa daraja ya kupata mali. Hali hii ni kinyume cha mambo yalivyo katika enzi hizi ambapo vijana wa kizazi cha *Gen Z* hupata mali mapema maishani kwa njia mbalimbali wala haijalishi iwapo wameelimika au hawajaelimika. Wengi wao hutajirika kupitia kwa vipawa walivyo navyo vya muziki, kuigiza, kufanya biashara ya sarafu za kigeni, kuunda maudhui mtandaoni na kufanya kazi nyinginezo zinazotokana na ujuzi walio nao ambazo huwapa mapato. Utajiri wao huja haraka na sio tu kwa kuelimika. Wamepoteza imani katika elimu kwa sababu imekosa kuwaondoa katika matatizo ya kiuchumi. Mazingira haya ndio yanayosababisha vijana kubadilisha methali hiyo ili iwiane na uhalisia wa mazingira ya enzi hizi.

### 4.1.3 Methali[2a]: Mtaka cha mvunguni sharti ainame

Hii ni methali ya kimapokeo ambayo kulingana na King'ei na Ndalu (2008) ina maana kwamba atakayekupata kitu ambacho kimefichika mvunguni, analazimika kuinama ili kukifikia kile kitu. Inatumiwa kumweleza mwenye haja fulani, hana budi kuishughulikia au kuitaabikia haja yake ili aitimize. Kihistoria, methali za kitamaduni za Kiafrika zilibeba busara na hekima yenye mamlaka kutoka kwa wazee. Kauli hii inashadidiwa na Fadare (2020) anapodai kwamba hata hivyo hekima hii inapingwa katika baada-methalijadi au kubuni upya methali hizo kwa kudunisha hekima iliyomo kimzaha.

Lyotard (1984) alitilia shaka imani zilizomo katika simulizi ambazo zinaonekana kueleza kuhusu mambo kwa mfano elimu huleta mafanikio, utamaduni haukosolewi, hekima huleta mali na kadhalika. Anahoji kwamba katika kipindi cha Baada-Usasa, kila mtu ana mtazamo wake kuhusu ukweli. Hakuna mtazamo mmoja wenye ukweli, kuna mitazamo mingi. Kinachoonekana kama ukweli kinategemea utamaduni, tajriba au mtazamo wa mtu binafsi kuhusu jambo husika. Kwa hivyo mitazamo mingi inaweza kuwepo kwa wakati mmoja.

Baada-methalijadi zinaakisi haya yote kwa sababu ni zao la kubadilishwa kwa muundo wa methali za kimapokeo, kujumuishwa kwa kejeli na mzaha pamoja na fasiri anuwai zinazojitokeza. Methali[2a] ina baada-methalijadi yake. Baada-methalijadi haziibuki katika ombwe tupu, Mieder (2004) anaunga mkono kauli hii na kueleza kwamba baada-methalijadi zinadumisha uhusiano wa kidayalojia baina yake na methali za kimapokeo. Hii inamaanisha kueleweka kwa maana za baada-methalijadi hutegemea vile hadhira inavyotambua muundo asilia wa methali husika ya kimapokeo huku ikiendelea kuifasiri upya katika miktadha ya sasa.

#### 4.1.4 Methali[2b]: Wahenga hawaamini mtaka cha mvunguni anaweza kukipata bila kuinama

Methali za kimapokeo ni semi fupi za moja kwa moja na zinazoelekeza mtu jinsi ya kuishi na watu. Methali[2b] iliyotokana na Methali[2a] imepanuliwa. Inaanza kwa kutoa ripoti kwamba *wahenga hawaamini*…na kufuatiwa na kifungu cha maneno kutoka katika methali asilia pamoja na maneno yaliyoongezwa hivyo kuipanua. Jambo hili, kwa mujibu wa Lyotard na Brugger (2001), maana za matamshi sio thabiti wala hazijabanwa katika umbo moja la jadi bali hufasiriwa upya na mazingira mapya ya kijamii na kitamaduni. Iyabode (2016) anakubaliana na mawazo ya Lyotard na Brugger anaposema baada-methalijadi kama miundo hubadilika inapobuniwa upya. Jambo hili linafafanuliwa zaidi na Raji-Oyelade (2020) anapokaulisha kwamba baada-methalijadi hupanua muundo asilia kwa kuongeza vifungu na vipengele vinavyofasiriwa upya. Omari (2016) anashadidia pia wazo hilo kwa kusema kwamba kifungu kilichoongezewa hujumuisha mawazo zaidi ya kizazi cha sasa na utamaduni. Hata hivyo, baada-methalijadi hudumisha elementi za methali za kimapokeo na kuziunda upya kwa kutumia mikakati maalum ya kiisimu, (Raji-Oyelade, 2023).

#### 4.1.5 Methali[3a]: Mchagua jembe si mkulima

Methali hii ni ya kimapokeo. Ni tamko fupi linalowashauri watu kutochagua kazi. Kuna hisia katika methali hii kwamba mtu anayechaguachagua kazi hana ujuzi wa kuifanya. Kwa mujibu wa Wamitila (2001), maana ya methali hii ni mkulima anayeifahamu barabara kazi yake hachagui jembe la kulimia. Anaeleza kuwa hutumiwa kutunasihi kwamba mtu mwenye nia ya kulifanya jambo fulani hulifanya bila ya kungojea udhuru wa aina yoyote ile.

#### 4.1.6 Methali[3b]: Wahenga hawaamini nimechagua jembe na nikalima

Hili toleo jipya la methali Methali[3a] limepanuliwa kimuundo na likayakinishwa kinyume na toleo asilia ambalo lilikanushwa. Hali hii inawiana na mawazo ya Lyotard (1984) kwamba simulizi zinazofahamika hutupiliwa mbali na maana kufasiriwa upya. Isitoshe tamko la toleo la kimapokeo ni fupi likilinganishwa na toleo la baada-methalijadi. Baada-methalijadi imerefushwa kwa kuongezwa maneno mawili zaidi. Hata hivyo hudumisha chembechembe za methali asilia lakini maana aghalabu hubadilika, kukejelishwa na kusasaishwa, (Ajadi na Oloruntoba-Oju, 2023). Wanasisitiza kwamba baada-methalijadi hutegemea muktadha na kuzielewa huhitaji maarifa ya methali asilia na muktadha wa sasa wa kijamii. Vijana wa kizazi cha *Gen Z* hutumia methali hii katika muktadha ambapo wanateua binafsi mambo yanayowafaa kisha wanayafanya na kufaulu. Kwa mfano wanaweza kupata nafasi nyingi za kazi na wakazipuuza kwa kuwa sio wanazotaka. Wanapochagua ile wanayotaka, huichangamkia na kuifanya vizuri sana. Hatimaye husema, ‘Wahenga hawaamini nimechagua jembe na nikalima.

#### 4.1.7 Methali[4a]: Tenda wema wende zako

Hii ni methali ya asilia ya kimapokeo. Ni tamko fupi lenye mamlaka ambalo linamshauri mtu yeyote anayemtendea mwenzake mema kwenda bila kutarajia shukrani. Kulingana na King’ei na Ndalu (2008), unapomfanyia mwenzako wema, usitegemee akulipe kwani mwanadamu hana wema. Mungu pekee ndiye hutulipa kwa wema wetu. Methali hii hushauri watu kuwa wanapowatendea wenzao wema hawafai kudai shukrani zao bali watende wema kama zawadi. Katika muktadha wa kitamaduni, watu walitarajiwa kutendeana mema bila kushukuriwa kwa kuwa waliamini Mungu angewalipa kwa wema waliotenda. Hawakutarajiwa kudai kulipwa au kushukuriwa kwa wema waliotenda.

#### 4.1.8 Methali[4b]: Nimetenda wema na nikasimama hapo, najua wanasikia kujinyonga

Hili ni toleo jipya la Methali[4a.] Kimuundo imepanuliwa kwa kuongezwa maneno. Pia inapinga methali asilia. Katika muktadha wa sasa, maana ya methali hii imebadilishwa na vijana wa kizazi cha *Gen Z* ili kukidhi mahitaji ya miktadha ya sasa kama anavyosema Owomoyela (2021) kwamba katika mazingira ya mijini, kidijitali na yenye msukumo wa kisiasa, watu huunda upya methali ili zikidhi hali halisi mpya. Isitoshe imejumuisha mzaha ambao ni mmojawapo wa mhimili wa nadharia ya baada-usasa kwa mujibu wa Lyotard (1984). Mzaha huo unatokea katika sehemu ya mwisho ya baada-methali katika maneno *‘najua wanasikia kujinyonga.’* Tofauti na methali ya kimapokeo, ambayo inawashauri watu kutenda wema na kwenda zao, baada-methalijadi hii inadai shukrani au malipo baada ya kutenda wema. Vijana katika muktadha wa sasa hudai malipo kwa kila wanalotenda, ni enzi za nipe nikupe, hakuna

cha bure. Hali hii ni kinyume kabisa cha matarajio ya jamii ya jadi, na uasi unadhihirika pia katika hii baada-methalijadi kama wanavyodai Ajadi na Oloruntoba-Oju (2023).

**4.1.9 Methali[5a]: Mpanda ngazi hushuka**

Methali mpanda ngazi hushuka ina maana kwamba, apandaye ngazi habaki juu milele bali huja wakati akateremka (King'ei na Ndalu, 2008). Kawaida watu wanaotumia kazi kupanda juu, hatimaye hushuka chini. Methali hii hutumiwa kukemea watu wanaofanikiwa kimaisha kwamba wasiwadharau wenzao walio chini kiuchumi kwa kuwa wanaweza kufilisika wakati wowote. Kimuundo, hii methali ni tamko fupi lenye wingi wa busara. Linawakumbusha watu walio na uwezo wa kiuchumi kutodharau watu kwa sababu mradi tu walipanda, wanaweza kushuka pia.

**4.1.10 Methali[5b]: Mpanda ngazi hushuka, mi sishuki, ju huku juu ndio nabaki**

Hii baada-methalijadi imebadilishwa kwa kuongezwa maneno. Hata hivyo bado maneno katika methali asilia iliyotokana nayo hayajapotea. Raji-Oyelade na Oyeleye (2019) wanahoji baada-methalijadi hutokana na methali za kimapokeo na mara nyingi hudumisha baadhi ya maneno, muundo ama vishazi funguzi huku maana zake zikibadilishwa. Kishazi kifunguzi 'Mpanda ngazi hushuka' ambacho ni methali asilia kimedumishwa kama anavyosema Saka (2024) kuwa baada-methalijadi nyingi hudumisha kishazi funguzi na kubadilisha maneno ya mwisho. Sifa ya ufupi wa tamko la methali ambayo hujitokeza katika methali nyingi za kimapokeo imepotea hapa pia kwani idadi ya maneno saba imeongezwa ilhali hayapo katika methali asilia. Hivyo muundo wa methali asilia umevurugika na imebadilika ikawa katika hali kanushi wala si yakinishi kama ilivyokuwa kabla ya mabadiliko. Hekima iliyomo katika methali asilia ni kwamba, maisha yana changamoto hivyo mafanikio hayadumu. Mpanda ngazi anaweza kushuka, hili linapingwa na vijana wa kizazi cha *Gen Z* wanaoidengua hekima hiyo kwa kupinga uwezekano wa kushuka baada ya kufanikiwa. Wazo hili linawiana na mawazo ya Lyotard (1984) ya nadharia ya baada-usasa. Kauli *'mi sishuki, ju huku juu ndio nabaki'* inaonyesha upinzani dhidi ya simulizi zinazofahamika katika jamii za jadi kuhusu kutodumu kwa mafanikio. Aidha, matumizi ya lugha ya mitaani kama *'mi'* na *'ju'* yanaonyesha michezo ya lugha inayohusishwa na baada-usasa, ambapo vijana hutumia ubunifu wa kiisimu kuunda utambulisho wao na kuwasilisha maana mpya zinazolingana na mazingira yao ya sasa ya kijamii na kidijitali. Katika muktadha wa sasa, vijana hutumia methali hii kwa maana kuwa mara tu wakishafanikiwa kimaisha, mafanikio hayo yanadumu. Wanaendelea kubaki huko juu, hali hii inadhoofisha hekima iliyomo katika methali za kimapokeo kama anavyodai Saka (2024).

**4.1.11 Methali[6a]: Siku njema huonekana asubuhi**

Iwapo siku itakuwa njema, inaweza kufahamika mapema asubuhi kwa kuona jinsi inavyoanza, (King'ei na Ndalu, 2008). Wanaeleza methali hii ina maana kwamba dalili za kitu au jambo au hali hujitokeza mapema. Methali za kimapokeo huwa na maana mbili; ya nje na ndani. Maana ya ndani ndio hubeba hekima ya methali ambayo hutumika katika muktadha mahsusi kuelimisha, kuonya, kutahadharisha, kushauri au kukemea. Baada-methalijadi huwa na maana moja, na maana zake hutokana na maana ya nje ya methali za kimapokeo. Mara nyingi huwa na kejeli, ucheshi, kinaya na stihizai, tofauti na methali za kimapokeo ambazo Finnegan (2012) anadai hueleza dhana za kidhahania kwa kutumia sitiari.

**4.1.12 Methali[6b]: Siku njema kwangu imeonekana jioni wahenga wanadhani ni AI**

Kama ilivyo sifa ya baada-methalijadi, methali hii imedumisha kifungu funguzi kilicho katika methali asilia. Hivyo tamko la methali hii humfanya msikilizaji akumbuke methali asilia ambayo imetokana nayo. Methali hii inahama kutoka katika ukweli wa kijumla hadi katika tajriba ya kibinafsi kupitia kwa istilahi *kwangu.* Hali hii inakiuka busara ya pamoja ya jamii iliyo katika methali za kimapokeo. Kauli hiyo inaungwa mkono na Ayinuola (2020) anapodai kwamba baada-methalijadi hupindua kauli zisizobadilika na busara ya hekima iliyomo katika methali za kimapokeo na kuunda methali mpya zilizo na maana za kibinafsi. Isitoshe wakati unabadilishwa kutoka asubuhi hadi jioni na kuashiria mafanikio yaliyocheleweshwa. Hali hii inaonyesha matumizi ya kinyume, kauli inayoshadidiwa na Raji-Oyelade (1999) aliyetambua kwamba baada-methalijadi hupinga au kukaidi methali za kimapokeo kwa kutumia vinyume vya maneno yaliyomo katika methali asilia na kuvuruga utaratibu wa maana zilizozoeleka.

Baada-methalijadi hii ina sehemu mbili, ya kwanza imedumisha maneno ya methali asilia na sehemu ya pili imebinafsishwa kwa matumizi ya neno *kwangu*, kinyume cha neno katika methali asilia kinajitokeza na mrejesho wa jamii unadhihirika kupitia kwa maneno '*wahenga wanadhani ni AI.'* Aidha matumizi ya istilahi *AI* yanadhihirisha mwingiliano wa methali asilia na teknolojia ya kisasa ili kunnda maana mpya zinazolingana na miktadha ya kiteknolojia.

Mseto wa lugha ya kiteknolojia na hekima ya simulizi za kitamaduni, Kulingana na Ayinuola (2020) ni jambo la kawaida katika diskosi za mitandao ya kijamii. Katika enzi hizi za Akili Ige *(AI)* watu wana uwezo wa kuzalisha picha na video na kuzipakua kwenye mitandao ya kijamii. Vijana

wengi wa kizazi cha *Gen Z* wamekuwa wakipakua mitandaoni video na picha zilizozalishwa kwa *AI* kuonyesha mafanikio yao. Hali hii ndio inayomfanya aliyetamka baada-methalijadi hiyo kusema kwamba *wahenga wanadhani ni AI*. Kuna hisia kwamba alipakua picha au video ya fanaka zake kwenye mtandao wa kijamii. Kwa hivyo anasema 'wahenga wanadhani ni *AI' ilhali si AI*, ni picha halisi za mafanikio yake. Hivyo siku njema kwake ilionekana jioni ilhali alifanikiwa kando na imani kwamba siku njema huonekana asubuhi.

**4.1.13 Methali[7a]: Mtaka yote hukosa yote**

Aliye na tamaa ya kupata kila kitu hafanikiwi kupata chochote (King'ei na Ndalu, 2008). Methali hii ina busara ya kitamaduni na hupigiwa watu walioshikwa na tamaa ya kupata kila kitu kwa wakati mmoja. Methali hii ya kimapokeo kama zilizvyo nyingi za kimapokeo ni fupi lakini ina utajiri wa hekima. Kauli hii inashadidiwa na Wanjala (2011) anayedai kuwa methali ni semi fupi zinazosheheni mafumbo juu ya ukweli wa maisha ya binadamu na huwa na umbo maalum. Umbo fupi lililogawika katika sehemu mbili, ya kwanza ikiwakilisha mtenda na kitendo na sehemu ya pili ikiwakilisha matokeo ya kitendo kwa hivyo kuna athari ya kisababu na kisababishi. Mieder (2004) anahoji kawaida methali husimba ukweli unaotokana na tajriba aliyo nayo mtu kupitia kwa miundo mifupi yenye kisababu na kisababishi.

**4.1.14 Methali[7b]: Mtaka yote hubeba yote**

Mabadiliko ya kitenzi hukosa hadi hubeba katika baada-methalijadi hii yanabadilisha mwelekeo wa kiitikadi na maana ilivyokuwa katika methali asilia. Methali asilia inaonya dhidi ya tamaa huku baada-methalijadi inayotokana nayo ikipendekeza uwajibikaji, uvumilivu na bidii. Muundo wa baada-methalijadi hii umetokana na methali ya kimapokeo iliyotokana nayo. Maneno ya kwanza ya methali ya kimapokeo '*mtaka yote*' yamehifadhiwa katika baada-methalijadi, mpangilio wa kisintaksia umedumishwa na neno '*yote'* limerudiwa katika matoleo ya methali zote. Mbinu hii ya mageuzi ni kipengele cha kawaida cha baada-methalijadi ambapo muundo wa jadi huhifadhiwa huku maana ikibadilishwa kupitia kwa ubadilishaji maneno (Raji-Oyelade, 2023). Mbinu hii inaruhusu wasikilizaji kutambua methali ya kimapokeo iliyotokana nayo. Kimuktadha, matumizi ya baada-methalijadi hii ni kinyume cha methali ya kimapokeo iliyotokana nayo. Methali ya kimapokeo inavunja watu moyo dhidi ya kujilimbikizia mali ilhali baada-methalijadi inawahimiza kutia bidii katika kazi zao ili wabebe vyote wanavyotaka. Hali hii inaakisi uhalisia wa sasa jambo ambalo Ayinuola (2020) anashadidia kwa kuhoji kwamba baada-methalijadi huakisi miktadha ya sasa ambapo watu hubuni njia anuwai za kutafuta kipato. Methali hii inaelekea kuonyesha kwamba wale wanaotaka yote ndio wanayopata yote.

**4.1.15 Methali[8a]: Mtegemea cha nduguye hufa maskini**

Hii ni methali ya kimapokeo na ina sifa zote za methali za kimapokeo zikiwemo ufupi, hekima ya jadi na vipande viwili vya kishairi ambavyo kimoja kinatoa wazo na kingine kulikamilisha. King'ei na Ndalu, (2008) wanasema maana yake ni mtu anayeshindwa kufanya kazi na badala yake kutegemea mali ya ndugu zake hubakia maskini. Ni muhimu tutegemee jasho letu, wala sio kuwa wavivu. Hekima ya jadi iliomo katika methali hii inahimiza uwajibikaji binafsi ambapo mtu anatoa mchango wake kwa jamii badala ya kuwa mzigo. Inakuza maadili ya kazi na kujitegemea pamoja kutahadharisha dhidi ya uvivu au kutegemea wanajamii wengine.

**4.1.16 Methali[8b]: Mtegemea cha nduguye hufa maskini na Oburu Odinga amechukua ODM**

Hii ni baada-methalijadi iliyotokana na methali ya kimapokeo *mtegemea cha nduguye hufa maskini*. Kama zilivyo sifa za baada-methalijadi, methali hii imehifadhi sehemu ya kwanza ya methali ya kimapokeo na kuipanua zaidi kwa kuongeza maneno yanayobadilisha maana iliyokusudiwa. Methali hii imechukua mkondo wa kibinafsi kama asemavyo Ayinuola (2020) kwamba ubunilizi wa baada-methalijadi hutegemea miktadha inayoakisi uhalisia wa sasa. Hivyo huzifanya zifasiriwe kwa mitazamo ya kibinafsi alimradi anayefasiri awe na ufahamu wa methali ya kimapokeo iliyotokana nayo. Kisintaksia, baada-methalijadi hii ina muundo wa sentensi ambatano ambapo sentensi mbili sahili zimeunganishwa kwa kiunganishi *na*. Kipande cha pili cha methali kimetokana na muktadha wa kisiasa nchini Kenya ambapo Oburu Odinga, nduguye marehemu Raila Amolo Odinga alichukua uongozi wa chama cha *Orange Democratic Movement* baada ya kifo chake. Hivyo baada-methalijadi hii inapinga methali asilia. Huku methali asilia ikihimiza uwajibikaji kikazi na bidii ya watu binafsi, baada-methalijadi inaelekea kuonyesha kwamba mtu anaweza kuchukua chochote cha nduguye baada ya kifo chake. Hivyo haihimizi bidii ya mtu binafsi. Baada-mthalijadi hii pia ina ucheshi, mbinu ambayo hujitokeza katika aina hizi za methali kwa mujibu wa Raji-Oyelade na Oyeleye (2019). Oburu Odinga kuchukua uongozi wa chama cha ODM na hili kutokea katika kipera cha fasihi simulizi ni jambo la kuchekesha, hekima ya jadi imeunganishwa na siasa za sasa nchini Kenya.

## 5.0 Hitimisho

Kutokana na matokeo ya utafiti, imedhihirika dhahiri kwamba methali za kimapokeo zinaundwa upya ingawa umbo lake asilia halipotezwi. Sehemu moja huhifadhiwa na nyingine kubadilishwa au yote ikahifadhiwa na sehemu mpya kuongezwa ili kubadilisha maana. Imebainika pia kwamba ufasiri wa baada-methalijadi unategemea miktadha zinamotumiwa. Mara nyingi mwingiliano matini baina ya methali za kimapokeo na baada-methalijadi unatokea. Hivyo mwingiliano kati ya hekima ya jadi na masuala katika miktadha ya sasa inadhihirika. Matokeo haya yanaonyesha kwamba mabadiliko ya methali za jadi hayana budi kufanyika kwa sababu ya haja ya kutumia simulizi hizo lakini kwa njia zinazokidhi haja za kizazi cha sasa katika muktadha wa sasa. Isitoshe changamoto zilizopo sasa ni tofauti na changamoto zilizokuwepo katika enzi za jadi. Kwa hivyo simulizi zinabadilishwa ili kuakisi masuala mbalimbali katika miktadha ya sasa.

## Marejeleo


Adom, D., Chukwuere, J. E., Addo, I. A., Tabi-Agyei, E., Thulla, P. F. Y. (2021). African Proverbs for Cultural Education: A Step towards Digital Archiving. Journal of History Culture and Art Research, 10(4), 44-59. doi:http://dx.doi.org/10.7596/taksad.v10i4.3118F

Adeniyi, K. O., & Ojerinde, O. A. (2024). *Nigerian Pidgin postproverbials: A sociolinguistic analysis of social realities in selected NP postproverbials*. In A. Raji-Oyelade (Ed.), *Postproverbials at work: The context of radical proverb-making in Nigerian languages*. Pp 263-288. doi: https://naklada.ffos.hr/knjige/index.php/ff/catalog/book/26

Ajadi, R. A., and T. Oloruntoba-Oju. (2023). "CORPORA ISSUES IN PROTOPROVERBIALS AND POSTPROVERBIALS OF YORUBA CULTURE". *Proverbium - Yearbook*, vol. 40, no. 1, Pp. 1-24, doi:10.29162/pv.40.1.49.

Ayinuola, O. A. (2020). Linguistic Representations of Postproverbial Expressions among Selected Yoruba Speakers: A Socio-Cultural Interpretation. *Matatu*, *51*(2), 311-326. https://doi.org/10.1163/18757421-05102007

Egbara, C. C. (2020). Of Proverbs and Postproverbial (Re)Constructions: An Evaluation of 'Altering Alternatives' in Selected Igbo Proverbs. *Matatu*, *51*(2), 346-359. https://doi.org/10.1163/18757421-05102009

Fadare, N. O. (2020). *Postproverbial and postmodern aesthetics in Ify Asia Chiemeziem's new media proverbs*. *Matatu: Journal for African Culture and Society*, *51*(2), 254–271. https://doi.org/10.1163/18757421-05102003

Finnegan, R. (2012). Oral Literature in Africa. Open Book Publishers.

Heidegger, M. (1962). *Being and time* (J. Macquarrie & E. Robinson, trans.) Harper & Row.

Hutcheon, L. (1988). *A poetics of postmodernism: History, theory, fiction*. Routledge.

Iyabode, O.A.D. (2016). Proverbs and Modernity: Taking the proverbs out of the mouth of the elders. Proverbium 33: 1-14.

Kim, G. W., Vaswani, R., Kang, W., Nam, M., & Lee, D. (2017). Enhancing ecoliteracy through traditional ecological knowledge in proverbs. Sustainability, 9, 1182. doi:10.3390/su9071182.

King'ei, K. na Ndalu, A. (2008). *Kamusi ya Methali*. EAEP.

Lyotard, J. F. (1984). *The postmodern condition: A report on knowledge* (Vol. 10). University of Minnesota Press.

Lyotard, J. F., & Brügger, N. (2001). What about the Postmodern? The Concept of the Postmodern in the Work of Lyotard. *Yale French Studies*, (99), 77-92.

Mieder, W. (2004). *Proverbs: A handbook*. Greenwood Press.

Nietzsche, F. (1968). *On the genealogy of morality* (W. Kaufmann & R. J. Hollingdale, trans.). Vintage International.

Nnabuihe, C. N. O. C. B. (2024). Postproverbials In Igbo: An Anthropo-Linguistic Overview. In A. Raji-Oyelade (Ed.), *Postproverbials at work: The context of radical proverb-making in Nigerian languages*. Pp89-117.

Ogbebor O. (2011). The value of indigenous knowledge system based on literature review [Blog post]. http://osarome.blogspot.com/2011/12/write-on-value-of-indigenous- knowledge.html [23.06.2024].

Ojiakor, C. T. (2024). *Igbo postproverbials: The dynamic act of the cultural deviant*. In A. Raji-

Oyelade (Ed.), *Postproverbials at work: The context of radical proverb-making in Nigerian languages*, Pp. 153–175.

Omari, S. (2016). Swahili modern proverbs: the role of literary writers and social network users. In *Swahili Forum* (Vol. 23).

Owomoyela, O. (2021). *Proverbs and African modernity: Defining an ethics of becoming*. **Yoruba Studies Review, 2**(2), 1–15. https://doi.org/10.32473/ysr.v2i2.130132

Raji-Oyelade, A., & Oyeleye, O. (2019). *Introduction: The postproverbial agency: Texts, media and mediation in African cultures*. *Matatu: Journal for African Culture and Society, 51*(2), 229–240 https://doi.org/10.1163/18757421-05102001

Raji-Oyelade, A. (1999). *Postproverbials in Yoruba culture: A playful blasphemy*. *Research in African Literatures, 30*(1), 74–82. https://doi.org/10.2979/RAL.1999.30.1.7

Saka, I.O. (2024). On Lexico-Semantic Analysis of Yoruba Deviant Proverbs. In International Journal of Language and Linguistics. Vol. 12, Issue 6. Pp 194-205

https://doi.org/10.11648/j.ijll.20241206.11

Wanjala, F.S. (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi*. Serengeti Educational Publishers Ltd.